Imetolewa tarehe: 26 Agosti, 2010

MAMLAKA YA CHAKULA NA DAWA

MAELEZO YA UTANGULIZI YA KAIMU MKURUGENZI MKUU WA TFDA, BW. HIITI B. SILLO KATIKA MKUTANO WA WAANDISHI WA HABARI KUHUSU MATOKEO YA OPERESHENI MAMBA III KATIKA UKUMBI WA MAMLAKA YA CHAKULA NA DAWA, TAREHE 26 AGOSTI 2010

Mkurugenzi wa Makosa ya Jinai (DCI), Kamishna wa Polisi Bw Robert Manumba,

Mwakilishi wa Katibu Mkuu, Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii,

Mkuu wa INTERPOL, Tanzania, Kamishna Msaidizi wa Polisi Bw Hussein Laisseri

Mwakilishi wa Mkurugenzi Mkuu, Idara ya Usalama wa Taifa,

Mwakilishi wa Mkurugenzi Mkuu, Tume ya Ushindani (FCC),

Mwakilishi wa Kamishna wa Ushuru na Forodha (TRA),

Wakurugenzi wa Mamlaka ya Chakula na Dawa,

Wanahabari,

Wafanyakazi wenzangu,

Mabibi na Mabwana,

Naomba nichukue fursa hii kwa niaba ya wafanyakazi wa TFDA kuwakaribisha, katika ofisi za Mamlaka ya Chakula na Dawa. TFDA ni taasisi iliyo chini ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii yenye jukumu la kudhibiti ubora na usalama wa vyakula, dawa, vipodozi na vifaa tiba.

Naamini wote tunaelewa dhima ya TFDA ambayo ni kulinda afya za wananchi kwa kuzuia athari zinazoweza kujitokeza kutokana na matumizi ya bidhaa tunazozidhibiti yaani vyakula, dawa, vipodozi na vifaa tiba. Hata hivyo, moja ya changamoto tunayokabiliana nayo katika shughuli ya udhibiti ni uwepo wa bidhaa bandia na duni kwenye soko la Tanzania.

Ndugu wanahabari,

Tumewaalika ili kuwapa taarifa juu ya Operesheni Mamba III iliyofanywa na Mamlaka ya Chakula na Dawa, Jeshi la Polisi nchini na Shirikisho la Polisi wa Kimataifa (Interpol). Operesheni hii imeshirikisha pia taasisi zingine ambazo ni TAMISEMI, Tume ya Ushindani (FCC), Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Ofisi ya Rais, Bohari Kuu ya Dawa (MSD) na Kitengo cha Huduma za Dawa cha Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii.

Operesheni imefanyika katika mikoa sita (6) ya **D**ar es Salaam, Arusha, Mbeya, Dodoma, Shinyanga na Mwanza katika vipindi viwili yaani tarehe 8-9 Julai 2010 na 28-29 Julai 2010. Operesheni ilishirikisha watendaji 80 kutoka katika taasisi hizi.

Napenda pia kuwafahamisha kwamba Operesheni hii imefanyika pia katika nchi za Kenya, Uganda, Rwanda, Burundi na pia Tanzania Visiwani katika tarehe tofauti za mwezi Julai chini ya uratibu wa INTERPOL.

Ndugu wanahabari,

Operesheni hii ni mwendelezo wa Operesheni Mamba zilizowahi kufanyika nchini katika kipindi cha mwezi Septemba 2008 na Agosti 2009. Kama ilivyokuwa katika Operesheni za awali, lengo la

Operesheni hii lilikuwa ni kukamata na kuwafikisha katika vyombo vya sheria wale wote wanaojihusisha na biashara ya dawa bandia.

Dawa zilizolengwa zilikuwa ni dawa za kutibu ugonjwa wa malaria, viuavijasumu (antibiotics), dawa za kuongeza nguvu za kiume - jamii ya Viagra na dawa za kupunguza maumivu - jamii ya "Paracetamol". Dawa hizi zilichaguliwa kutokana na kuwa na matumizi makubwa zaidi hapa nchini na hivyo kuwa na soko kubwa kiasi cha kuvutia biashara haramu ya dawa bandia.

Ndugu wanahabari,

Katika mikoa niliyoitaja Operesheni hii ilifanyika katika maeneo yafuatayo; wilaya zote tatu za mkoa wa Dar es Salaam, Arusha mjini, Namanga, Mbeya mjini, Tunduma, Shinyanga mjini, Kahama, Mwanza mjini, Geita, Dodoma mjini na pia Zanzibar. Maeneo yaliyokaguliwa ni pamoja na yale ya biashara ya dawa ambayo ni famasi na maduka ya dawa baridi (DLBDs) maduka ya dawa muhimu (DLDMs), maghala ya kutunzia dawa, hospitali binafsi, zahanati, maeneo ya mipakani (ports of entry) na maeneo yote yaliyotiliwa mashaka ya kuwepo kwa dawa hizo bandia na zisizo kidhi viwango.

Ndugu wanahabari,

Napenda kuwataarifu kuwa kufuatia Operesheni Mamba zilizofanyika mwaka 2008 na 2009, hatua mbalimbali za kisheria zilichukuliwa kwa wote waliopatikana na dawa bandia na duni. Hatua hizo ni pamoja na kuwapa onyo wafanyabiashara wanane (8). Aidha, kesi 50 bado zipo katika hatua ya upelelezi katika mikoa ya Dar-es-Salaam (kesi 17), Mwanza (kesi 4), Shinyanga (kesi 5), Mbeya (kesi 4) na Arusha (kesi 20).

Ndugu wanahabari,

Mamlaka imeazimia kuendelea kushirikiana na vyombo vingine vya udhibiti hapa nchini **ikiwa ni pamoja na mradi wa WHO/IMPACT kwa kushirikiana na INTERPOL** katika kukabiliana na tatizo la dawa bandia ili kuwalinda wananchi dhidi ya madhara ya bidhaa

hizo bandia hususan chakula, dawa na vipodozi. Aidha, ni vyema kutambua kuwa biashara ya **dawa bandia ni biashara haramu inayovuka mipaka (cross-boarder crime),** inayohitaji juhudi zetu sote kama nchi na pia ushirikiano na nchi tunazopakana nazo kama ilivyofanyika katika operesheni hii.

Ndugu wanahabari,

Naomba nichukue nafasi hii kuwapongeza na kuwashukuru kwa dhati kabisa wale wote waliofanikisha Operesheni hii. Kipekee natoa shukrani kwa wakuu wa taasisi na watumishi wa Jeshi la Polisi Bohari Kuu ya Dawa (MSD), Tume ya Ushindani (FCC), Mamlaka ya Mapato (TRA), Ofisi ya Rais, Mikoa na Halmashauri zilizoshiriki, Kitengo cha Huduma za Dawa cha Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii na Kurugenzi ya Dawa na Vipodozi iliyoratibu Operesheni hii kwa upande wa Mamlaka ya Chakula na Dawa. Napenda pia kuvishukuru vyombo vyote vya habari kwa mchango mkubwa wa kutoa elimu kwa umma kuhusu kazi za udhibiti wa ubora na usalama wa bidhaa na vyakula, dawa, vipodozi na vifaa tiba.

Ndugu wanahabari,

Kabla ya kuhitimisha maelezo yangu, napenda kuwakumbusha wananchi ujumbe muhimu katika mapambano haya kuwa **"dawa bandia ni hatari kwa afya za binadamu na husababisha vifo".**

Baada ya maelezo haya ya utangulizi, napenda kuchukua fursa hii kumkaribisha Mkurugenzi wa Makosa ya Jinai nchini, Kamishna wa Polisi, Bw. Robert Manumba ili aweze kutoa matokeo ya Operesheni Mamba ya tatu.

Asanteni kwa kunisikiliza